FUNZO LA 20

1. Hata kama mababu wetu walimkataa Mungu, Je, Mungu aliacha mpango wake wa kutuma Mwokozi?
-La.

2. Kwa sababu mababu wetu walimkataa Mungu, Mungu alimchagua nani ambaye kupitia kwake angemtuma mwokozi?
-Abramu.

3. Je, Mungu alimchagua Abramu kwa sababu Abramu hakutenda dhambi?
-La.
-Abramu alikuwa mwenye dhambi.

4. Je, ni kwa nini Mungu alimchagua Abramu?
-Abramu aliamini kuwa dhambi yake ilistahili kifo.
-Abramu aliamini kuwa ni Mungu pekee ambaye alikuwa na uwezo wa kumwokoa.
-Abramu aliamini kuwa Mungu angemtuma Mwokozi.

5. Abramu alimuoa Sarai, walikuwa na watoto wangapi?
-Hakuna.

6. Je, ni kwa nini Abramu na Sarai hawakuwa na watoto?
-Kwa sababu Sarai alikuwa tasa.

7. Je, Mungu alimwambia Abramu afanye nini?
-Mungu alimwambia Abramu atoke katika nchi yake na aende katika nchi ambayo Mungu angemwongoza.



8. Mungu alinena na Abramu kupitia sauti yake. Je, Mungu hunena vipi na sisi siku hizi?
-Siku hizi, Mungu hunena nasi kupitia kwa Neno lake, Biblia yake.

9. Je, Mungu alimuahidi nini Abramu?
-Kwanza, Mungu alimuahidi kuwa uzao wake utakuwa mwingi na pia watakuwa watu wakuu.
-Pili, Mungu aliahidi kuwa atambariki.
-Tatu, Mungu alimuahidi kuwa atawabariki wale watakao mbariki, na kuwalaani wale watakao mlaani.
-Nne, Mungu aliahidi kuwabariki watu wote kupitia kwa mmoja wa uzao wa Abramu.

10. Je, ni nani huyo katika uzao wa Abramu ambaye kupitia kwake watu wote wangebarikiwa?
- Mwokozi.

11. Mwokozi angefanya nini?
-Mwokozi angekuja kuzishinda nguvu za dhambi.
-Mwokozi angekuja kuzishinda nguvu za kifo.
-Mwokozi angekuja kuzishinda nguvu za Shetani.
-Mwokozi angekuja kuwapatanisha watu na Mungu tena.

12. Je, ni nani huyo katika uzao wa Abramu ambaye kupitia kwake watu wote wangebarikiwa?
-Mwokozi.

13. Baada ya Mungu kumuahidi Abramu, Abramu alifanya nini?

-Abramu alitoka katika nchi aliokuwa akiishi, na akamfuata Mungu kuelekea nchi aliokuwa akimwelekeza.

14. Je, Mungu alimwelekeza Abramu wapi?
-Mungu alimwelekeza Abramu kwa nchi iitwayo Kanani.

-Je, unakumbuka Lutu alikuwa nani?

-Lutu alikuwa mpwa wa Abramu ambaye walienda naye Kanani.

-Siku moja, kulikuwa na tatizo kati ya Abramu na Lutu.

Tusome Mwanzo 13:5-7

5-Na Lutu aliyesafiri pamoja na Abramu, yeye naye alikuwa na makundi ya ng'ombe na kondoo, na hema.
6-Na ile nchi haikuwatosha, ili wakae pamoja; maana mali zao zilikuwa nyingi, hata wasiweze kukaa pamoja.
7-Kukawa ugomvi kati ya wachunga wanyama wa Abramu, na wachunga wanyama wa Lutu; na siku zile Wakanaani na Waperizi walikuwa wakikaa katika nchi.

-Je, tatizo kati ya Abramu na Lutu lilikuwa lipi?

-Abramu alikuwa na ng’ombe na kondoo wengi.
-Lutu pia alikuwa na ng’ombe na kondoo wengi.

-Lutu na Abramu walikuwa na ng’ombe na kondoo wengi na hawakuwa na sehemu ya malisho ya kutosha.



-Je, Abramu alifikiria nini ya kusuluhisha hilo tatizo?

Tusome Mwanzo 13:8-9

8-Abramu akamwambia Lutu, Basi, usiwepo ugomvi, nakusihi, kati ya mimi na wewe, wala kati ya wachungaji wangu na wachungaji wako; maana sisi tu ndugu.
9-Je! Nchi hii yote haiko mbele yako? Basi ujitenge nami, nakusihi; ukienda upande wa kushoto, nitakwenda upande wa kuume; ukienda upande wa kuume, nitakwenda upande wa kushoto.

-Abramu alifikiria kuwa yeye na Lutu watengane.
-Abramu alifikiria kuwa Lutu achague sehemu yake ya kuishi.

-Kama Lutu angechagua mabondeni, basi Abramu angeishi milimani.

-Kama Lutu angeishi milimani, Abramu angeishi mabondeni.
-Wacha tusome alichochagua kufanya Lutu:

Tusome Mwanzo 13:10-11

10-Lutu akainua macho yake, akaliona Bonde lote la Yordani, ya kwamba lote pia lina maji, kabla Bwana hajaharibu Sodoma na Gomora, lilikuwa kama bustani ya Bwana, kama nchi ya Misri hapo unapokwenda Soari.
11-Basi Lutu akajichagulia Bonde lote la Yordani; Lutu akasafiri kwenda upande wa mashariki; wakatengana wao kwa wao.

-Lutu alichagua mabondeni.
-Je, ni kwa nini Lutu alichagua mabondeni?

-Kwa sababu kulikuwa na nyasi ya kutosha kuwalisha ng'ombe na kondoo wake.

-Lutu alikuwa akifikiria kuhusu nyasi pekee.
-Lutu alikuwa akifikiria kuhusu ng'ombe na kondoo wake wengi.

-Lutu alikuwa akifikiria kuhusu utajiri wake.
-Lutu alifanya uamuzi mbaya kuishi mabondeni.

-Je, kwa nini Lutu alifanya uamuzi mbaya?

-Kwa sababu Lutu hakumuuliza Mungu afanye nini.
-Kwa sababu Lutu alikataa kumsikiliza Mungu.

-Kaini alikataa kumsikiliza Mungu na akamuua ndugu yake Habili.

-Kizazi cha Kaini kilikataa pia kumsikiliza Mungu.
-Kizazi chote cha Kaini kilikufa katika mafuriko.

-Je, nini kitakachofanyika tukikataa kumsikiliza Mungu?

-Tukikataa kumsikiliza Mungu, tutakufa.

-Tukikataa kumsikiliza Mungu, tutaenda katika Ziwa la Moto wa Milele ambalo liliandaliwa Shetani na mapepo wake.



-Je, ng'ombe, mbuzi au utajiri mkubwa waweza kutuokoa kutokana na Ziwa la Moto wa Milele?
-La.

-Lutu alikataa kumsikiliza Mungu, akahamia mabondeni.

Tusome Mwanzo 13:12-13

12-Abramu akakaa katika nchi ya Kanaani, na Lutu akakaa katika miji ya lile Bonde; akajongeza hema yake mpaka Sodoma.
13-Lakini watu wa Sodoma walikuwa wabaya, wenye kufanya dhambi nyingi sana juu ya Bwana.

-Mabondeni, kulikuwa na miji miwili.
-Majina ya hiyo miji ilikuwa ni Sodoma na Gomora.

-Watu wa Sodoma na Gomora hawakumwamini Mungu.
-Watu wa Sodoma na Gomora walikuwa waovu sana.

-Je, Mungu aliuona uovu wa watu wa Sodoma na Gomora?
-Ndiyo.

-Je, twaweza kuficha chochote tunachofikiri kutoka kwa Mungu?
-La.

-Je, twaweza kuficha chochote tunachosema kutoka kwa Mungu?
-La.

-Je, twaweza kuficha chochote tunachofanya kutoka kwa Mungu?
-La.

-Je, Mungu alimwambia nini Abramu baada ya Lutu kuhamia mabondeni?

Tusome Mwanzo 13:14-15 & 17

14-Bwana akamwambia Abramu, alipokwisha kutengana na Lutu, Inua sasa macho yako, ukatazame kutoka hapo ulipo, upande wa kaskazini, na wa kusini na wa mashariki na wa magharibi;
15-maana nchi hii yote uionayo, nitakupa wewe na uzao wako hata milele.
17-Ondoka, ukatembee katika nchi hii katika mapana yake, na marefu yake, maana nitakupa wewe nchi hiyo.

-Mungu alimuambia Abramu kuwa atampa ardhi ya Kanani.

-Pia Mungu alimwambia Abramu:

Tusome Mwanzo 15:5-6

5-Hapo Mwenyezi-Mungu akamleta Abramu nje na kumwambia, “Tazama mbinguni! Zihesabu nyota, kama kweli utaweza kuzihesabu! Hivyo ndivyo wazawa wako watakavyokuwa wengi!”
6-Abramu akamwamini Mwenyezi-Mungu, naye Mwenyezi-Mungu akamkubali Abramu kuwa mwadilifu.



-Mungu alimwambia Abramu pia kuwa uzao wake utakuwa mwingi kama nyota.

-Je, kuna nyota ngapi?
-Zaidi ya kuhesabika.

-Ingawaje Abramu hakuwa na watoto, Mungu alimwambia kuwa uzao wake utakuwa mwingi kama nyota.

-Ingawaje Abramu hakuwa na watoto, je, Abram alimwamini Mungu?
-Ndiyo.

-Abramu aliamini kuwa siku moja Mungu angempa mtoto.

-Abramu aliamini kuwa mmoja wa uzao wake angekuwa Mwokozi ambaye angewaokoa watu.

-Pia Mungu alimwambia Abramu:

Tusome Mwanzo 15:13-16

13-Bwana akamwambia Abramu, Ujue hakika ya kwamba uzao wako utakuwa mgeni katika nchi isiyo yake, watawatumikia watu wale, nao watateswa muda wa miaka mia nne.
14-Hata na taifa lile, watakaowatumikia, nitawahukumu; baadaye watatoka na mali mengi.
15-Lakini wewe utakwenda kwa baba zako kwa amani, utazikwa katika uzee mwema.

16-Na kizazi cha nne kitarudi hapa, maana haujatimia uovu wa Waamori bado.

-Mungu alisema kuwa uzao wa Abramu utaishi katika nchi nyingine, na baada ya miaka 400, Mungu atawarejesha Kanani.

-Je, Mungu alijuaje kile kingefanyikia uzao wa Abramu?

-Mungu alijua kile kingefanyika kwa uzao wa Abramu kabla wazaliwe.

-Je, unajua nini kitakachofanyika kesho?
-La.

-Je, wajua nini kitakachofanyika mwezi ujao?
-La.

-Je, wajua nini kitakachofanyika mwaka ujao?
-La.

-Lakini Mungu anajua kila kitu.

-Mungu anajua kitakacho tufanyikia kesho.
-Mungu anajua kitakacho tufanyikia mwezi ujao.
-Mungu anajua kitakacho tufanyikia mwaka ujao.

-Mungu anajua kitakachofanyika usoni.

-Abramu alipofika miaka 99, Mungu alinena naye tena.



Tusome Mwanzo 17:1-5

1-Abramu alipokuwa mtu wa miaka tisini na kenda, Bwana akamtokea Abramu, akamwambia, Mimi ni Mungu Mwenyezi, uende mbele yangu, ukawe mkamilifu.
2-Nami nitafanya agano langu kati ya mimi na wewe, nami nitakuzidisha sana sana.
3-Abramu akaanguka kifudifudi. Mungu akamwambia, akasema,
4-Mimi, agano langu nimefanya nawe, nawe utakuwa baba wa mataifa mengi,
5-wala jina lako hutaitwa tena Abramu, lakini jina lako litakuwa Ibrahimu, kwani nimekuweka uwe baba wa mataifa mengi.

-Mungu alinena na Abramu na akampa jina mpya.

-Je, jina mpya alilopewa Abramu na Mungu ni lipi?
-Ibrahamu.

-Je, kwa nini Mungu alimpa Abramu jina mpya?

-Kwa sababu Abramu angekuwa na uzao mwingi.

-Pia Mungu alimpa Sarai jina mpya.

Tusome Mwanzo 17:15-16

15-Mungu akamwambia Ibrahimu, Sarai mkeo, hutamwita jina lake Sarai, kwa sababu jina lake litakuwa Sara.

16-Nami nitambariki, na tena nitakupa mwana kwake, naam, nitambariki, naye atakuwa mama wa mataifa, na wafalme wa kabila za watu watatoka kwake.

-Je, jina mpya alilopewa Sarai na Mungu ni lipi?
-Sara.

-Je, kwa nini Mungu alimpa Sarai jina mpya?
-Kwa sababu Sarai angekuwa na uzao mwingi.

-Ingawaje Sara alikuwa mzee sana na tasa, Mungu aliahidi nini?

-Ya kuwa Sara atakuwa mama wa uzao mwingi.
-Ya kuwa Sara atazaa mwana.

-Tusome alichofanya Abramu baada ya Mungu kumuahidi:

Tusome Mwanzo 17:17

17-Ndipo Ibrahimu akaanguka kifudifudi akacheka, akasema moyoni, Je! Mtu wa umri wa miaka mia, kwake atazaliwa mtoto? Naye Sara mwenye umri wa miaka tisini atazaa?

-Je, Ibrahamu na Sara walikuwa na miaka mingapi?
-Ibrahamu alikuwa na miaka 100 na Sara alikuwa na miaka 90.

-Je, Ibrahamu alicheka kwa nini?

-Je, Ibrahamu alicheka kwa sababu hakumwamini Mungu?



-La.

-Je, ni kwa nini Ibrahamu alicheka?

-Ibrahamu alicheka kwa sababu yeye na Sara walikuwa wazee, na Mungu alikuwa anaenda kuwapa mwana.

-Je, Ibrahamu na Sara walikuwa na miaka mingapi?
-Ibrahamu alikuwa na miaka 100 na Sara alikuwa na miaka 90.

-Je, Mungu angeweza kumpa mzee wa miaka 100 na mkewe wa miaka 90 mtoto?
-Ndiyo.

-Je, ni nani aliyeumba mtu wa kwanza?
-Mungu.

-Je, ni nani aliyeumba mwanamke wa kwanza?
-Mungu.

-Je, ni nani humpa kila mtoto uhai?
-Mungu.

-Je, kuna chochote ambacho Mungu hawezi kufanya?
-La.

-Mungu anaweza pia kumpa mzee wa miaka 100 na mkewe wa miaka 90 mtoto.